



OFFICE OF THE DEPUTY PRINCIPAL
ACADEMICS, RESEARCH AND STUDENT AFFAIRS

UNIVERSITY EXAMINATIONS

2020/2021 ACADEMIC YEAR

FIRST YEAR SECOND SEMESTER REGULAR EXAMINATION

**FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF
EDUCATION ARTS**

COURSE CODE: KIS 120

**COURSE TITLE: INTRODUCTION TO KISWAHILI
LITERATURE**

DATE: 26TH JULY, 2021

TIME: 8.00AM – 11.00AM

INSTRUCTION TO CANDIDATES

- SEE INSIDE

THIS PAPER CONSISTS OF TWO PRINTED PAGES

PLEASE TURN OVER

REGULAR- MAIN EXAM

KIS 120: INTRODUCTION TO KISWAHILI LITERATURE

STREAM: B. ED (ARTS)

DURATION:3HOURS

Maagizo kwa watahiniwa

- i. *Jibu swali la KWANZA na mengine MAWILI.*
- ii. *Majibu YOTE yaandikwe kwenye karatasi maalum ya majibu.*
- iii. *Mtihani huu una jumla ya maswali MATANO.*

Swali la Kwanza

- a. Eleza sifa TANO zinazotofautisha fasihi Simulizi na fasihi andishi (Alama 10)
- b. 'Mhakiki wa kazi za fasihi ana mchango mkubwa kwa taifa lake'. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea vipengele VITANO. (Alama 10)
- c. Kwa kutumia hoja TANO, eleza jinsi mtunzi wa 'Kilio cha Haki' anaendeleza maudhui ya dhuluma. (Alama 10)

Swali la Pili

Huku ukirejelea riwaya ya 'Tumaini', jadili mambo MATANO ambayo mhakiki wa riwaya hujishughulisha nayo. (Alama 20)

Swali la Tatu

- a. Fafanua dhana ya 'ngomezi'. (Alama 4)
- b. Huku ukirejelea hoja NNE, eleza umuhimu wa nyiso katika jamii. (alama 8)
- c. Eleza sifa NNE za ngano katika fasihi Simulizi. (Alama 8)

Swali la Nne

- a. Tathmini tofauti kati ya mashairi huru na mashairi ya arudhi. Zingatia hoja TANO (Alama 10).
- b. Kwa kutumia mifano MITANO jadili muundo wa shairi la arudhi. (Alama 10)

Swali la Tano

Fafanua ujumbe unaojitokeza katika shairi lifuatalo:

Ajabu

Ajabu ajabu hii ajaabu

Mwenye maneno hasemi

Asonayo anasema

Na nyuma hawatazami

Mbele wamekuandama.

Ajabu ajabu hii ajabu

Wanaolima hawali

Wasolima wanakula

Hula viso halali

Nguvu pia na fadhila.

Ajabu ajabu hii ajabu

Wachokao hawalali

Walalao ni wazima

Hulala pema pahali

Na hulku wakikoroma.

Ajabu ajabu hii ajabu

Watendao si muhimu

Wasotenda watukufu

Wao ni watu adhimu

Kila siku twasifu.

Ajabu ajabu hii ajabu

Mwenye haki si wa haki

Asonacho hunguruma

Kwa uhuru na miliki

Mwenye haki humtuma.